

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/AGOSTI 2018

MUDA: SAA 2 ½

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI KIDATO CHA 4**

MAAGIZO

1. Jibu maswali **manne** pekee.
2. Swali la kwanza ni la **lazima**.
3. Kisha chagua maswali mengine **matatu** kutoka sehemu zilizosalia.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. Kila swali lina alama 20.

**SEHEMU YA A – RIWAYA: KIDAGAA KIMEMWOZEA**  
**SWALI LA LAZIMA**

1. “Wema wako umeniua kabisa, kuna mahakama ndani ya moyo wangu, ninajishtaki mwenyewe kila siku kwa miaka na mikaka”.
- (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)  
(b) Onesha mbinu zozote mbili zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)  
(c) Thibitisha ukweli wa kauli kuwa mnenaji wa maneno haya si mtu bali ni hayawani. (alama 12)

**SEHEMU YA B – TAMTHILIA: KIGOGO**  
**Jibu swali la 2 au 3**

2. “Dalili ya mvua ni mawingu, lazima tuwe macho”.
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)  
(b) Bainisha tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)  
(c) Ushauri uliotolewa na msemaji baadaye kama njia mojawapo ya kuwa macho ni wa kidhalimu. Fafanua. (alama 4)  
(d) Eleza namna unafiki wa msemaji na upumbavu wa mnenewa unavyodhihirika katika muktadha wa dondoo hili. (alama 6)  
(e) Onesha jinsi ukweli wa kauli hii ulivyojitokeza baadaye katika tamthilia. (alama 4)
3. Jadili migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya *kigogo*, kisha utathmini namna ilivyosuluhishwa. (alama 20)

**SEHEMU YA C: HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA**

**Jibu swali la 4 au 5**

4. “Kesho kama sote tutaamka salama.....kama tutafungua milango ya nyumba zetu”....
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)  
(b) Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)  
(c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)  
(d) Hadithi hii inaakisi mambo mengi yanayotendeka katika bara la Afrika.  
Taja mambo sita (alama 6)
5. Ukengeushi huzorotesha maendeleo ya kijamii. Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya ‘Mkubwa’. (alama 20)

**SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI**

6. (a) Eleza vipengele **vitano** vya fasihi simulizi ambavyo hujitokeza katika fasihi andishi. (alama 10)
- (b) Fafanua sifa **tano** za ushairi simulizi. (alama 10)

**SEHEMU E: USHAIRI**

**7. Soma mashairi haya kisha ujibu maswali yanayofuata.**

**Shairi A**

Umekata mti mtima  
Umeangukia nyumba yako  
Umeziba mto hasira  
Nyumba yako sasa mafurikoni  
Na utahama  
Watoto kuwakimbia.

Mbuzi kumkaribia chui  
Alijigeuza panya  
Akalia kuliwa na paka kichwani  
Mchawi kutaka sana kutisha  
Alijigeuza samba  
Akalia na risasi kichwani.

Jongoo kutaka sana kukimbia  
Aliomba miguu elfu  
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa utakwenda  
Bwanako kumpa sumu?  
Hadija umemshika nyoka kwa mkia,  
Hadija umepita nyama ya Punda.

**Shairi B**

Piteni jamani, Piteni haraka  
Nendeni, nendeni huko mwendako  
Mimi haraka, haraka sina,  
Mzigo wangu, mzigo mzito mno  
Na chini sitaki kuweka.

Vijana kwa nini hampiti?  
Kwa nini mwanicheka kisogo?  
Mzigo nilioubeba haupo kichwani  
Lakini umenipinda mgongo na miguu  
Na lazima nijiegemeze, kichwani  
Chini nendeko.

Haya Piteni! Piteni! Haraka! Heei!  
Mwafikiri mwaniacha nyuma!  
Njia ya maisha ni moja tu  
Huko mwendako ndiko nilikotoka  
Na nilipofikia wengine wenu  
Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema  
Niko nyuma ya wakati  
Lakini kama mnepita mbele  
Na uso wangu kuutazama  
Ningewambia siri ya miaka mingi.

### **MASWALI**

- (a) Haya ni mashairi ya aina gani? (al.1)
- (b) Washairi hawa wawili wanalalamika. **Yafafanue** malalamishi yao. (al.4)
- (c) Onesha vile kinaya kinavyojitokeza katika tungo hizi mbili. (al.6)
- (d) Kwa kurejelea shairi 'B' **eleza** maana ya: (al.3)
- (a) mzigo
- (b) Siri
- (c) Niko nyuma ya wakati
- (e) **Andika** ubeti wa kwanza wa shairi 'A' kwa lugha nathari (alama 4)
- (f) Uhuru wa mshairi umetumiwa vipi katika shairi 'B' (alama 2)